


# FANYENI YOTE KWA JINA LA YESU KRISTO

Mchungaji Denis & Devis Julius

## YALIYOMO

Utangulizi…………………………………………………………………………………3

Uhalali wa kulitumia jina Yesu………………………………………………………..4

Namna ya kulitumia jina la Yesu…………………………………………… ……..4

Mifano ambayo jina la Yesu lilitumika kuhudumu…………………………..……..6

Aina ya Sala na Jina la Yesu,………………………………………………………………..7

Igizo…………………………………………………………………………………………7

Nyimbo…………………………………………………………………………………….8

Ujumbe kwa Wazazi…………………………………………………………………..8

Hitimisho……………………………………………………………………………………..9

Mawasiliano…………………………………………………………………………...9

**MAFUNDISHO MAALUMU KWA WATOTO.**

**Utangulizi:**

Huu ni mfufulizo wa miongozo ya mafundisho maalumu, kwa ajili ya Watoto, Kwa msaada wa miongozo mingine iliyotangulia, wasiliana nasi kwa namba hizi +255 693 036 618. Au kwa email. Info@wingulamashahidi.org.

Katika mwongozo huu, Mtoto atajua maana ya kufanya mambo yote katika jina la Yesu Kristo. Na hiyo ndio nyenzo kuu, tuliyopewa na Mungu kutusaidia katika mambo yetu yote. Wewe kama mzazi au mlezi ukizingatia kumzoesha mtoto kulitaja jina la Yesu (mahali panapastahili), Basi utamlinda na mengi, na mitego mibaya ya ibilisi. Kumbuka mtoto asipofundishwa kuiishi ndani ya jina hili, basi ataishi katika jina la shetani.

Darasa hili ni fupi, hivyo tumia  wiki moja au mbili, kuwafundisha, na kuwahakiki.

Bwana akubariki.

## Uhalali wa kulitumia jina la Yesu:

Biblia inasema;

Wakolosai 3:17

> *17 Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye.*

Hilo ni agizo ambalo tumepewa na Mungu kwamba mambo yetu yote tuyafanye katika jina la Yesu Kristo,  Mpaka tumepewa agizo hilo, Maana yake ikiwa hatutafanya kwa jina hilo, ni wazi kuwa  kuna hatari inaweza kuzalika aidha  ya kukosea tunachotaka kukifanya , au kupoteza, au kuangamia kabisa..

Hivyo Ikiwa sisi tuna ujuzi wa kuyatenda mambo yote katika jina hilo hatuna budi pia kuwafundisha Watoto wetu mapema, namna ya kusimama na jina  hili kuu tangu wakiwa wadogo.

## Namna ya kulitumia jina la Yesu:

Sasa Kutenda katika jina la Yesu kama inavyotajwa hapo, kulilengwa kwa namna mbili;

1. Ni kufanya mambo yote katika maagizo ya Yesu, yaani sawasawa na yale Yesu aliyotufundisha.
2. Lakini pia kulitumia jina la Yesu kama nyenzo katika maeneo kadha wa kadha mfano maombi, maombezi, sala, kubariki.

### 1] Maana ya kwanza: Kufanya mambo yote katika maagizo ya Yesu.

Yaani sawasawa na yale Yesu aliyotufundisha,. Wewe kama Mwalimu, Wafundishe “HOFU YA KRISTO“kwa Kuwaambia kabla hawajaongea Neno lolote watafakari Je! Yesu analipenda neno hilo, Je! Limekubaliwa na Biblia?

Waambie yanayotoka kinywani kama vile matusi, uongo, majibizano, mizaha, masengenyo, hayatokani na jina ( agizo) la Yesu. Hivyo wajiepushe nayo kwasababu yatawakosesha uzima wa milele.

Sambamba na hilo wafundishe pia si tu maneno bali pia katika matendo yao, yanapaswa yawe kama Yesu anavyotaka. Waambie vitendo kama, Wizi, uchafu, kiburi, utundu, ukorofi, kupigana, dharau, kutokutii wazazi, Yesu hayaruhusu. Na hivyo vitawasababishia kukosa pia uzima wa milele.

Kama Mwalimu Wafundishe kusema na kukiri kwa vinywa vyao: “Sisi Ni Watoto wa Mungu, hatutaruhusu vinywa vyetu au matendo yetu kumkosea Mungu”

**2] Maana ya Pili: Kutumia jina la Yesu kama Nyenzo:**

Wafundishe, kwamba Kutenda katika jina la Yesu ni Pamoja, na kutumia jina la Yesu katika

Sehemu zifuatazo.

1) <u>Chakula:</u> kabla ya kula au kunywa kitu chochote wakibariki, Na kumalizia kwa kulitaja jina la Yesu Kristo
2) <u>Unapoomba hitaji lako lolote kwa Mungu:</u> mwishoni litaje pia kwa kusema ninaomba haya katika jina la Yesu Kristo
3) <u>Unapokemea nguvu za shetani:</u> kemea kwa jina la Yesu, labda wameota ndoto mbaya, au wanapoona hatari isiyo ya kawaida.
4) <u>Unapoombea wagonjwa:</u> au madhaifu taja jina la Yesu.
5) <u>Unapoingia mahali popote:</u> Labda shuleni, hospitalini, kwa wageni, kimoyo-moyo, waseme ninapatakasa mahali hapa kwa jina la Yesu, naufuta kila mkakati uliopangwa na adui kinyume changu.

Hii ni kuonyesha mamlaka anayoitumia inatoka moja kwa moja kwa Yesu Kristo, na hivyo atapokea anayoyataka bila tashwishwi yoyote tofauti na akiomba tu hivyo hivyo bila rejea ya jina.

Watoto wanapaswa wazoezwe sana, kulitaja jina la YESU mara kwa mara, katika mambo yaliyo ya msingi.

**Mifano ya maeneo jina la Yesu lilitumika Kuhudumu:**

Ipo mifano kadha wa kadha, kwenye biblia inayotuonyesha, baadhi ya vitu kufanywa kupitia jina la Yesu, Ifuatayo ni mifano hiyo;

<u>Kutoa Pepo:</u>

Luka 10:17

> *17 Ndipo wale sabini waliporudi kwa furaha, wakisema, Bwana, hata pepo wanatutii kwa jina lako*

Matendo 16:18

> *18 Akafanya hayo siku nyingi. Lakini Paulo akasikitika, akageuka akamwambia yule pepo, Nakuamuru kwa jina la Yesu Kristo, mtoke huyu. Akamtoka saa ile ile.*

<u>Walitumia jina la Yesu katika kuponya.</u>

Matendo 3:6-7

> *6 Lakini Petro akasema, Mimi sina fedha, wala dhahabu, lakini nilicho nacho ndicho nikupacho. Kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, simama uende.*
> *7 Akamshika mkono wa kuume, akamwinua, mara nyayo zake na vifundo vya miguu yake vikatiwa nguvu*

- Hivyo wewe kama Mwalimu wafundishe (kwa kuwaelewesha na kuwakaririsha) Watoto Sala ya Chakula, inayoishia na jina la Yesu.

- Sala ya Asubuhi, na Sala ya usiku kabla ya kulala inayomalizika na jina la Yesu.

**Aina ya Sala na Jina la Yesu**

**Sala ya Chakula.**

*Asante Mungu, kwa kunipa chakula hiki, ninaomba ukibariki, na kukitakasa, ninapokitumia kikanijenge mwili na nitie nguvu ya kukutumika vema, Na wale ambao hawajapata ninaomba ukawapatia kwa neema yako, Ni katika jina la Yesu Kristo ninaomba haya. Amen.*

**Sala ya Asubuhi.**

*Mungu wangu ninakushukuru kwa kunipa Zawadi ya siku nyingine mpya, asante kwa uzima na neema, ninaomba ninapoiendea mkono wako uniongoze nikatende na kuishi sawasawa na mapenzi yako yote, Walinde wazazi wangu na ndugu zangu, watembee katika mafanikio na amani, ninaomba haya katika jina la Yesu Kristo Amen.*

**Sala Ya Usiku.**

*Baba asante, kwa kutembea nami kutwa nzima ya leo, Ninaomba unisamehe dhambi zangu, nilizokutenda kwa kuwaza, kwa kunena, na Kutenda, ninaomba ninapokwenda kulala, unilinde usiku wote, niote ndoto njema, awatume Malaika zako kunifunika, Ninaomba haya nikiamini, katika jina la Yesu Kristo Amen*.

**IGIZO**

Igizo ni njia nyingine, bora ya kuwafundisha Watoto.

Watengezee igizo, labda mmoja wao anaumwa Kichwa, Halafu mmoja anakwenda kumwekea mikono na kusema "Ninaamuru maumivu ya Kichwa ondoka sasa katika jina la Yesu".

Halafu yule mmoja anasema nimepona, anashangalia na kufurahi.

Mwingine aigize kama ameanguka mapepo. Kisha mwingine anamfuata na kusema ninakuamuru wewe Pepo mtoke huyu kwa jina la Yesu Kristo. Halafu yule mwenzake anamka amepona.

Mwingine anataka kula chakula, bila kuomba, mmoja anamwambia, si vema ule chakula bila kukibariki kwa jina la Yesu, hivyo embu tuombe kwanza (anaombea chakula), na mwishoni anasema Baba ninakushukuru, kwa kuwa umekibariki chakula hiki ninaomba na kuamini katika jina la Yesu Kristo. Amen

## WIMBO

Wafundishe pambio: Au wimbo/nyimbo zenye maudhui zinazoelezea nguvu na mamlaka iliyo ndani ya jina la Yesu.

Mfano.

Pambio: …Jina la Yesu ni ngome yangu x2..Nitamkapo jina hilo ngome nyingine sina x2….

Tenzi No5: Jina lake Yesu, tamu tukilisikia.

Wimbo wa Kuabudu: Nalipenda jina hili Yesu x3,..jina lako lina nguvu, Yesu x3.

## UJUMBE KWA WAZAZI/ WALEZI:

Wafundishe Watoto kutoa ujumbe kwa wazazi wao au walezi, maana hao ndio waangalizi wao na wasimamizi wao wa siku zote

Waseme kwa Pamoja mbele ya kanisa maneno haya;

Wazazi tufundisheni na kutuzoeza kuyatenda mambo yote katika jina la Yesu Kristo.

Amen.

**Hitimisho**

Watoto wakifundishwa kuwa na hofu ya Kristo katika kila jambo, vilevile kutumia jina la Yesu kama silaha yao Madhubuti ya vita, utawakuza katika ushujaa na ujasiri ambao Kristo anautaka. Hakikisha unarudia madarasa haya mara kwa mara.

**MAWASIILIANO.**


Kanisa la Nuru ya Upendo

Wachungaji: Denis Julius & Devis Julius

Simu: +255 693 036 618 / +255 789v001 312

Email: info@ wingulamashahidi.org

Webisite: wingulamashahidi.org/